



KUZUIA WADUDU Toleo, TPC 2

Vikugu

(*Aphids, Family Aphididae*)

Vikugu hunawiri katika sehemu za dunia zisizo na jua kali wala baridi (Temperate). Hata hivyo vikugu vyaweza pia kupatikana katika sehemu za hari na zile za baridi.

Mahasimu

Vikugu huvamia miti ya kila aina, hasa sehemu changa. Kwa wingi vikugu huvamia vibweta-kunde (*legumes*), tikiti, tango nyasi na machungwa.

Dalili


Vikugu huvuta majimaji yaliyo kwenye sehemu changa na hatimaye kufanya matawi kujipinda. Aina ya jamii fulani ya vikugu hutoa mate yaliyo na sumu na kufanya mmea kukauka. Vikugu vya jamii nyingine hutoa aina fulani ya majimaji yanayo wavutia wadudu wengine, hivyo basi kusababisha hasara zaidi.

Baadhi ya vikugu pia hueneza viini vya magonjwa kama vile *bean mosaic virus*, *rosette virus* na *cucumber mosaic virus*. Aina moja ya jamii ya vikugu yaweza kueneza zaidi ya virusi 100 kwa zaidi ya mimea 30 ya jamii tofauti.

Kutambua

Vikugu ni wadudu wadogo wa mviringo. Rangi yao hutegemea jamii tofauti kama vile manjano, kijani, hudhurungi, kijivu, nyeupe na nyeusi.

Sehemu ya mdomo imechongoka ili kudunga kwenye sehemu za mimea na kunyonya. Vikugu huishi kwa pamoja katika sehemu changa za mimea.



Uvamizi wa vikugu

Kizazi

Kila kikugu kilicho komaa chaweza kuzaa kati ya vikugu 2 hadi 20 kwa siku moja. Katika hali iliyo sawa vikugu waweza kuishi kwa wiki mbili. Vikugu waweza kuwa na mabawa au kukosa.

Kuzuia na Kukabili

Hali mbaya ya hewa huweza kuangamiza vikugu, kama vile upepo mkali unao ambatana na mvua. Iwapo ni bustani ndogo waweza kuvinya vikugu kwa mkono au kukata zile sehemu zilizovamiwa na vikugu au hata kunyunyizia sehemu hizo

na maji ya sabuni. Tumia sabuni ya aina ya *potash* inayotumiwa kuosha vyombo wala sio sabuni zilizo na *caustic soda* inayodhuru mimea.

Chungu na sisimizi wapaswa kukabiliwa kwani huvutia vikugu na kuzuia mahasimu wa vikugu. Waweza kuzuia chungu na sisimizi kwa kutumia vizingiti au kwa kunyunyiza dawa iliyotayarishwa kutoka kwa tururu, *rhubarb* (*Rheum hybridum*) na nyanya. (Maelezo zaidi yaweza kupatikana kutoka kwa HDRA.)

Mimea yenye Afya: Miche yenye afya huhimili vikugu. Tumia mbolea ya boji ili kukuza mimea yenye afya. Mbolea za kisanisia huzalisha mimea iliyo na wingi wa majimaji yanayovutia vikugu. Aina mbalimbali ya mimea katika mfumo wa kuambatanisha mimea husaidia katika kukabili vikugu.

Kuambatanisha mimea: Kwa kuambatanisha mimea kama kitunguu saumu, *chives* (*Allium schoenoprasum*), tururu, *nasturtiums* (*Tropaeolum sp.*), *parsley* (*Petroselinum crispum*), mbaazi, vitunguu, *basil* (*Ocimum basilicum*) na *fennel* (*Foeniculum vulgare*), husaidia katika kukabili vikugu.

Mtego wa mimea: Aina ya mfumo huu hujumuisha ukuzaji wa aina ya mimea unaovutia vikugu. Hivyo basi vikugu huvamia mimea huu. Kwa mfano *milkweed* (*Asclepias sp.*), *sowthistle* (*Sonchus sp.*) na *black nightshade* (*Solanum nigrum*) huvutia vikugu na kupunguza hasara kwa mimea mingine.

Wadudu wenye manufaa: Kuna aina mbalimbali ya wadudu wanaohisimu vikugu. Mahasimu hawa wapaswa kukaribishwa kwa kuwacha mazingira yaliyo na mandhari hai. Baadhi ya mahasimu hao ni *hoverfly larvae* (*Syrphidae*), *ladybirds* (*Coccinellidae*), *lacewing larvae* (*Chrysopidae*, *Sisyridae*, *Hemerobiidae* & *Coniopterygidae*), nyigu, *praying mantis* (*Mantis religiosa*), ndege wadogo na buibui.

Mkojo wa ng'ombe: Ili kukusanya mkojo wa ng'ombe (au mbuzi na kondo) weka ndoo mahali sakafu ya zizi inapoteremka ili mkojo ukusanywe usiku. Wacha mkojo kwa wiki mbili kwenye jua. Fifisha mkojo huo kwa sehemu 1 ya mkojo na sehemu 6 za maji. (Mkojo usiofifishwa waweza kuchoma sehemu changa za mimea).

Unga: Tayarisha vikombe 2 vya unga uliochanganywa na maji lita 5 hadi 10. Nyunyiza asubuhi ili jua la mchana likaushe unga huo. Vikugu hubaki kwenye unga uliokauka na hatimaye kukauka.

Dawa za Kunyunyiza

Pilipili (*Capsicum frutescens*): Tumia 100g za pilipili, lita 1 ya maji na maji ya sabuni (tumia sabuni ya *potash* kama ile ya kuosha vyombo na wala sio zile za unga zilizo na *caustic soda* inayodhuru mimea). Pondaponda pilipili na kuongeza maji kisha kuvuruga. Chuja mchanganyiko huu na kufifisha kwa sehemu 1 ya mchanganyiko na sehemu 5 za maji ya sabuni.

Tahadhari: Mchanganyiko wa pilipili na viungo vya pilipili husababisha mwasho na harara ya ngozi.

Mtokoma mwitu (muvulu), mstafeli, (*Annona muricata*) *A. reticulata*, mtomoko, mtopetope (*A. squamosa*): Mtokoma mwitu hujulikana pia kama Muvulu *soursop*, *custard apple* au *sweetsop*. Chuna matunda mabichi kutoka kwa mmea huu kisha kupondaponda ili kutoa yale mafuta. Fifisha kwa maji kisha kunyunyizia. Waweza pia kukausha mbegu kisha kusaga na kunyunyiza moja kwa moja au kuongeza sehemu 20 za maji, na kunyunyiza.



Mtokoma mwitu (*Annona squamosa*)



Mwarobaini (*Azadirachta indica*): Mti huu ulitokea sehemu za India, Mwarobaini umesambaa sehemu nyingi za dunia kama bara Hindi na Afrika. Mbegu zaweza kupatikana kwa urahisi. Mbegu huokotwa kisha kukaushwa. Wakati unapohitaji kutayarisha dawa, utapondaponda mbegu hizo kisha kulowesha kwa siku moja. Tumia 2 hadi 50g ya unga wa mbegu kwa lita moja ya maji. Nyunyiza mchanganyiko huu kwenye mimea iliyoadhiriwa

Mwarobaini

Waweza pia kutumia mchanganyiko wa mkurubuku (*derris*), kitunguu saumu, *quassia* na tururu. Maelezo zaidi yaweza kupatikana kwa kuandikia HDRA, anwani imeandikwa hapa chini.

This update: Jan 2005

Tafsiri na: **Patrick Bunyali Kamoyani, September 2004. Maragoli Kenya.**

Email pbkamoyani@lycos.co.uk or pbkamoyani@excite.com

Tel +254-(0)-721 612 607

HDRA- Kwa huduma za kilimo hai, Ryton Organic Gardens Coventry, CV8 3LG, UK
Simu +44 (0)24 7630 3517 Kipepesi +44 (0)24 7663 9229 Barua pepe: ove-enquiry@hdra.org.uk
Mtandao: <http://www.hdra.org.uk>

Makala haya ni mkusanyiko wa utafiti wa kisayansi na maarifa ya kilimo hai. Maelezo haya sio bayana na viwango vya kimataifa kuhusu kilimo hai. Maelezo ya ziada kuhusu mbinu za kilimo hai yaweza kupatikana kutoka kwa HDRA. Waweza kunakili makala haya kwa sababu zisizo za kifaida. Shukrani ni kwa Charlton Community Development Trust kwa mchango wa kutayarisha makala haya.